TANGAZO LA SERIKALI NA.675 La Tarehe 21/8/2020

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(SURA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetungwa chini ya vifungu vya 7(1) na 16(1))*

## SHERIA NDOGO ZA ADA NA USHURU ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE ZA MWAKA 2020

Jina — **1**. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Wilaya Rungwe za Mwaka 2020.

Tafsiri — **2**. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:

"ada" maana yake ni yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni mtumishi wa umma yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia Sheria Ndogo hii;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe;

"kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"soko" maana yake ni ni eneo au soko liliotengwa na linalomikiwa na Halmashauri kama soko;

"ushuru" maana yake ni maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri;

"Wakala" maana yake ni kampuni iliyoteuliwa kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hii.

Utozaji wa ada na ushuru — **3.-** (1) Halmashauri itatoza ada na ushuru kwa ajili ya vibali, leseni na huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1), ada zinazototozwa chini ya Sheria Ndogo hii zitalipwa kwa Halmashauri.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1), ushuru

unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hii utalipwa kwa Halmashauri au Wakala wa Halmashauri kwa kadri Halmashauri itakavyoelekeza.

Wajibu wa kulipa ada na ushuru

**4.** Mtu yeyote anayestahili kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii atatakiwa kulipa ada au ushuru huo kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

Muda wa kukusanya ada na ushuru

**5.-** (1) Muda wa kukusanya ada na ushuru utakuwa ni kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni.

(2) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), Halmashauri au Wakala, kwa kibali cha Mkurugenzi, anaweza kukusanya ada au ushuru baada ya muda uliotajwa hapo juu.

(3) Malipo ya ada na ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii yatalipwa kwa Halmashauri au Wakala wake na kutolewa stakabadhi ya kielektroniki ya Halmashauri kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

Usimamizi wa Sheria Ndogo

**6.-** (1) Halmashauri inaweza kufunga biashara au kusimamisha uendeshaji wa shughuli yoyote ambayo itafanyika bila ya kuwa na leseni au kibali kinachotolewa na Halmashauri.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), Halmashauri au Wakala wake anaweza kukamata na kuzuia mali au bidhaa za mtu yeyote ambaye ameshindwa kulipa ushuru kwa mujibu wa masharti ya Sheria Ndogo hii.

(3) Endapo mmiliki wa mali au bidhaa iliyokamatwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) atashindwa kulipa ushuru unaodaiwa ndani ya siku saba kwa mali au bidhaa zisizoharibika haraka na ndani ya siku mbili kwa mali au bidhaa zinazoharibika haraka, Halmashauri, baada ya kupata amri ya Mahakama, itakuwa na mamlaka ya kuuza mali au bidhaa na fedha zitakazopatikana zitarejeshwa kwa mmiliki wa mali au bidhaa hizo baada ya kutoa ada au ushuru unaodaiwa, gharama za kuhifadhi mali au bidhaa, gharama za Mahakama na gharama za mnada.

(4) Wakala hataruhusiwa kukamata mali au bidhaa bila kupata idhini ya maandishi ya Mkurugenzi.

(5) Halmashauri haitawajibika kwa uharibifu wa bidhaa au mali iliyokamatwa chini ya kifungu hiki isipokuwa tu kama uharibifu huo umesababishwa na Halmashauri au Wakala.

Uteuzi wa Wakala

**7.-** (1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteua kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria kukusanya ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) atakuwa na wajibu wa:

(a) kukusanya na kupokea ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoidhinishwa katika Sheria Ndogo hii;

(b) kukusanya ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Mamlaka ya Afisa Mwidhiniwa

**8.** Bila kuathiri masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hii, Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo, jengo au chombo cha usafiri kwa nia ya kukusanya ada au ushuru, kufanya tathmini au kufanya jambo lolote linalohusu ada, ushuru, leseni au kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Makosa na adhabu

**9.-** (1) Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo atashindwa kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii na endapo atatiwa hatiani atahukumiwa adhabu ya faini isiyozidi shilingi elfu hamsini au kifungo kisichozidi miezi mitatu isipokuwa tu kama atathibitisha kuwa kushindwa kulipa ada au ushuru kumetokana na sababu zilizo nje ya uwezo wake.

(2) Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo:

(a) atamshawishi mtu au kundi la watu kukwepa au kukataa kulipa ada au ushuru; au

(b) atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au Wakala kuhusu huduma zinazohitaji kibali au leseni ya Halmashauri au shughuli zinazohitaji kulipiwa ushuru,

na endapo atatiwa hatiani atahukumiwa adhabu ya faini isiyozidi shilingi elfu hamsini au kifungo kisichozidi miezi mitatu au vyote kwa pamoja.

(3) Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo atamzuia Mkurugenzi, Afisa Mwidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii na endapo atatiwa hatiani atahukumiwa adhabu ya faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne.

Kufifilisha kosa

**10.** Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kiasi cha shilingi elfu thelathini kwa makosa yaliyoainishwa katika kifungu cha 9(1) na (3) na shilingi laki moja kwa kosa lililoainishwa katika kifungu cha 9 (3) endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi na kutimiza wajibu wake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Kufutwa Tangazo la

**11.** Sheria Ndogo za ada na ushuru za Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe za Mwaka 2011 zimefutwa.

Serikali
Na. 56 la
Mwaka
2012

JEDWALI LA KWANZA
*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 3(1))*

SEHEMU YA KWANZA
ADA YA NYUMBA NA VIBANDA VYA HALMASHAURI

| A: ADA ZA NYUMBA ZA MAKAZI | | |
|---|---|---|
| NA. | ENEO | KIWANGO CHA ADA |
| 1. | Daraja la Kwanza | Shilingi 80,000/= kwa mwezi |
| 2. | Daraja la Pili | Shilingi 50,000/= kwa mwezi |
| 3. | Daraja la Tatu | Shilingi 25,000/= kwa mwezi |
| | | |
| B: VIBANDA VYA BIASHARA | | |
| Na. | ENEO | KIWANGO CHA ADA |
| 1. | Soko Kuu | Shilingi 50,000;- hadi 70,000/= kwa mwezi |
| 2. | Stendi Mpya | Shilingi elfu 50,000/= hadi 70,000/= kwa mwezi |
| 3. | Tandale | Shilingi 30,000/= kwa mwezi |
| 4. | Katumba | Shilingi 10,000 hadi 20.000/= kwa mwezi |
| 5. | Tukuyu Mjini | Shilingi 20,000/=kwa mwezi |
| 6. | Soko la Mpuguso. | Shilingi 30,000/= hadi .50,000/= kwa mwezi |
| 7. | Soko la Kiwira | Shilingi 30,000/= hadi 50,000/= kwa mwezi |
| 8. | Ukumbi wa Halmashauri | Shilingi 200,000/= kwa siku |
| 9. | Huduma ya vyoo | Shilingi 200/= kwa mtu mmoja |
| 10. | Majengo mengine ya Halmashauri | Shilingi 20,000/= hadi 70,000/= kwa mwezi |

SEHEMU YA PILI

USHURU WA MASOKO NA MAENEO MENGINEYO NDANI YA HALMASHAURI

| Na. | AINA YA BIDHAA | KIWANGO CHA USHURU |
|---|---|---|
| 1. | Nyanya, Vitunguu, karoti na viungo vyote vya mboga | Shilingi 200 kwa siku |
| 2. | Mbogamboga na Matunda | Shilingi 200 kwa siku |
| 3. | Robota la mitumba | Shilingi 200 kwa siku |
| 4. | Kuku/Bata | Shilingi 200 kwa siku |
| 5. | Bidhaa za viwandani | Shilingi 200 kwa siku |
| 6. | Samaki | Shilingi 200 kwa siku |
| 7. | Jamii ya mikunde | Shilingi 200 kwa siku |
| 8. | Nafaka zote | Shilingi 200 kwa siku |
| 9. | Aina zote za viazi | Shilingi 200 kwa siku |

| | | |
|---|---|---|
| 10. | Ndizi aina zote | Shilingi 200 kwa siku |
| 11. | Mazao ya nafaka na mbegu | Shilingi 200 kwa siku |
| 12. | Kuuza na kuchoma nyama mnadani | Shilingi 1,500 kwa siku |

SEHEMU YA TATU

ADA ZA HUDUMA ZA MACHINJIO NA UKAGUZI WA NYAMA

| Na. | MNYAMA | KIWANGO CHA USHURU |
|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | Kwa bei ya kilo moja ya nyama |
| 2. | Mbuzi | Kwa bei ya kilo moja ya nyama |
| 3. | Nguruwe | Kwa bei ya kilo moja ya nyama |
| 4. | Kondooo | Kwa bei ya kilo moja ya nyama |

SEHEMU YA NNE

USHURU WA MADINI YA UJENZI

| Na. | AINA YA MADINI | KIWANGO CHA USHURU |
|---|---|---|
| 1. | Ushuru wa mchanga | Shilingi 1,000/= kwa Tani moja |
| 2. | Ushuru wa mawe | Shilingi 1,000/= kwa Tani moja |
| 3. | Ushuru wa Tofali za kuchoma | Shilingi 1,000/= kwa Tani moja |
| 4. | Ushuru wa Makaa ya mawe | Shilingi 5,000/= kwa Tani moja |
| 5. | Ushuru wa marumaru | Shilingi 2,000/= kwa Tani moja |
| 6. | Ushuru wa Chokaa | Shilingi 2,000/= kwa Tani moja |
| 7. | Ushuru wa kokoto | Shilingi 1,000/= kwa Tani moja |

SEHEMU YA TANO

USHURU WA NGOZI

| Na. | AINA YA MIFUGO | KIWANGO CHA USHURU |
|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | Shilingi 200/= kwa kila ngozi moja |
| 2. | MbuzI | Shilingi 200/= kwa kila ngozi moja |
| 3. | Kondoo | Shilingi 200/= kwa kila ngozi moja |
| 4. | Wanyama wengine | Shilingi 200/= kwa kila ngozi moja |

SEHEMU YA SITA

USHURU WA MAGULIO

| Na. | AINA YA WAFANYABIASHARA | KIWANGO CHA USHURU |
|---|---|---|
| 1. | Wauza Bia na Soda, wauza vyombo vya nyumbani, wauza vipuli vya baiskeli au vipuli vya magari, vipuli vya pikipiki, wauza madawa ya mifugo na binadamu | Shilingi 500/= kwa siku |
| | Wauza nguo mpya za dukani, wauza mitumba, viatu, wauza pombe za kienyeji, wauza vyakula na wenye vyerehani | |
| | Watengeneza baskeli na wauza madawa ya asili | |
| | Wauza samaki, nyama, chumvi, miwa, Matunda, karoti na viungo vyote vya mboga | |
| | Bidhaa nyingine ambazo hazijatajwa | |

SEHEMU YA SABA
USHURU WA KUSAFIRISHA MIFUGO NA SAMAKI

| Na. | AINA YA MFUGO | KIWANGO CHA USHURU |
|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe: | |
| | (a) Ndani ya Wilaya | Shilingi 1000/= kwa ng'ombe |
| | (b) Nje ya Wilaya | Shilingi 1500/= kwa ng'ombe |
| 2. | Mbuzi: | |
| | (a) Ndani ya Wilaya | Shilingi 1000/= kwa mbuzi |
| | (b) Nje ya Wilaya | Shilingi 1500/= kwa mbuzi |
| 3. | Kondoo: | |
| | (a) Ndani ya Wilaya | Shilingi 1000/= kwa kondoo |
| | (b) Nje ya Wilaya | Shilingi 1500/= kwa kondoo |
| 4. | Nguruwe: | |
| | (a) Ndani ya Wilaya | Shilingi 1000/= kwa nguruwe |
| | (b) Nje ya Wilaya | Shilingi 1500/= kwa nguruwe |
| 5. | Kuku/bata | |
| | (a) Ndani ya Wilaya | Shilingi 300/= kwa kuku/bata |
| | (b) Nje ya Wilaya | Shilingi 400/= kwa kuku/bata |
| 6. | Samaki | Shilingi elfi 2000 @ ndoo ya lita 20 |

SEHEMU YA NANE
ADA YA VIKUNDI

| Na. | AINA YA ADA | KIWANGO CHA ADA |
|---|---|---|
| 1. | Ada ya Kikundi | Shilingi 10,000/= kwa mwaka |
| 2. | Ada ya usajili wa kiundi | Shilingi 30,000/= |

SEHEMU YA TISA
USHURU WA MAZAO YA BAHARI, MITO, MAZIWA NA MABWAWA

| Na. | AINA YA ZAO | KIWANGO CHA USHURU |
|---|---|---|
| 1. | Samaki | Asilimia 3 ya bei ya zao |
| 2. | Mazao mengine | Asilimia 3 ya bei ya zao |

SEHEMU YA KUMI
USHURU WA MAZAO YA MISITU

Aina ya zao kiwango cha ushuru

(a) Kuni………………………………………………Tsh. 5,000/= kwa tani moja

(b) Mkaa
(i) Gunia moja la kg 35 …….……………….... Tsh. 2,000/= kwa gunia moja
(ii) Uuzaji mkaa rejareja ……………………………...…Tsh. 300/= kwa siku

(c) mbao- bila kujali unene ……………...…...…...…. Tsh.200/= kwa ubao mmoja

(d) nguzo-bila kujali unene na aina ya mtiTsh................................ 300/= kwa Nguzo
(e) fito- bila kujali unene na aina ya mti…......................Tsh.300/= kwa ufito mmoja
(f)Ushuru wa banzi moja..........................................................Tshs 100/= kwa banzi
(g) magogo bila kujali unene na aina ya miti …...........……Tsh. 1,000/= kwa gogo
(h) Nguzo za umeme ..................................................Tshs. 1,500/= kwa kila Nguzo

(i) Asali

(i) Nyuki wakubwa…………………….…………......500 kwa lita moja
(ii) Nyuki wadogo………………………..………………800 kwa lita moja

(j) Magogo "meter" yanayotumika viwandani kwa ajili ya nishati ya moto……………………………………….………….... Tsh. 35,000/= kwa tani
(k) Ushuru wa Nyungo…………………….………………. Tshs 50/= kwa ungo

SEHEMU YA KUMI NA MOJA
USHURU WA USAFIRISHAJI WA MAZAO

Kiwango cha ushuru

(a) Ndizi ……………………………...…... Tsh 300/= kwa mkungu,
  i. Gari ya Tani 1-3……….………...……......Tshs. 33,500/=
  ii. Gari ya Tani 4 -6 ……….….……………..... Tshs. 60,000/=
  iii. Gari ya Tani 7-9 …………….…………..…. Tshs. 120,000/=
  iv. Gari ya Tani 10-12 …………….…….………Tshs. 180,000/=
  v. Gari ya Tani 13 na kuendelea …….…...…...…Tshs. 335,000/=
  vi. Magari yanayosafirisha ndizi nje ya nchi ……... Tshs. 30,000/= kwa tani.

(b) Viazi………………. Tsh 2,000/= kwa gunia moja lenye uzito wa Kilogram 100 na gunia chini ya Kilogram 100 litalipiwa 1000/=
(c) Nanasi…………………………...………… Tsh 10,000/= kwa tani moja
(d) Embe…………………………………………. Tsh 2,000/= kwa gunia moja
(e) Parachichi…………………….…….………… Tsh 2,000/= kwa gunia moja
(f) Parachichi yanayosafirishwa nje ya nchi……. Tshs. 20,000/= kwa tani moja
(g) Mahindi makavu……………………………… Tsh 2,000/= kwa gunia moja
(h) Mahindi mabichi …………………………... Tshs. 10,000/= kwa tani moja
(i) Maharage na aina yote ya kunde…………... Tsh 2,000/= kwa gunia moja
(j) Vitunguu…………………………………....... Tsh 2,000/= kwa gunia moja
(k) Magimbi……………………………………...Tsh 2,000/= kwa gunia moja
(l) Machungwa……………………………….… Tsh 2,000/= kwa gunia moja
(m) Mihogo……………………………………...Tsh 2,000/= kwa gunia moja
(n) Mafyulisi………………………………………. Tsh 2,000/= kwa gunia
(o) Aina nyingine zote za matunda ambazo hazijaainishwa………. Tsh 2,000/= kwa gunia moja
(p) Mazao mengine ambayo hayajaainishwa……... Tsh 2,000/= kwa gunia moja mfano Tangawizi, hiriki n.k
(q) Ushuru wa miwa …………………………………. Tshs. 15,000/= kwa tani

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 10)*

KUFIFILISHA KOSA

Mimi…………………………………………. nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya …………………………ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe kuwa tarehe ………mwezi………. Mwaka………. nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha………………. cha Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ya Mwaka 2020.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, nipo tayari kulipa shilingi ……………………………. na kutimiza wajibu wangu chini ya Sheria Ndogo hiyo badala ya kushtakiwa mahakamani.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI KWELI NA NINAYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe……………. ya Mwezi…………………..…. Mwaka……………………

Jina………………………………………Saini……………………………………

Mbele ya:

Jina……………………………………...Cheo…………………………………….

Saini……………………………………Tarehe…………………………………...

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hii kufuatia Azimio la Mkutano Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe uliofanyika tarehe ………... mwezi…………… 2019 katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe.
Mbele ya Wafuatao:-

…………………………
Mhe. Ezekiel M. Mwakota
Mwenyekiti (W)Halmashauri Wilaya
Rungwe

…………………………………..
Bi. Loema I. Peter
*Mkurugenzi Mtendaji (W)*
*Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe*

S.L

NAKUBALI

Dodoma ,
Tarehe…. /…….2020

MHE. SELEMANI SAID JAFO
*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais*
*Tawala za Mikoa na Serikali*
*Za Mitaa (TAMISEMI)*